

FEBRUARI 2019 | NAMBA 22

# MAMBO MUHIMU


*Chapisho la kila Robo, la Ofisi ya Tawi ya Ellen White Estate - Adventist University of Africa*

# UTATU WA KIMBINGU

Utatu wa Kimbingu katika Maandishi ya Ellen White 2

Sura Inayomtambulisha Mungu 3

Utatu 6



*Tunautaka ukweli kwa kuwa ni ukweli, na tunaukataa uongo kwa sababu ni uongo*

# UTATU WA KIMBINGU KATIKA MAANDISHI YA ELLEN WHITE

**Anna Galeniece**

## HISTORIA USULI

Teolojia ya Waadventista iliyojengwa juu ya Biblia haikugunduliwa na kuanzishwa kwa siku moja. Ilichukua miaka kadhaa kuendelezwa. Kwa mfano, fundisho la hekalu halikueleweka kikamilifu na kukubalika Oktoba 23, 1844, siku Hiram Edson alipopokea uelewa wa kwanza wa hekalu la mbinguni, siku iliyofuata tu ya Kukatishwa Tamaa Kukuu. Ilichukua idadi ya miaka kutoka 1844 hadi mwishoni mwa 1860, hadi Waadventista walipouelewa kikamilifu uzuri wa ujumbe wa hekalu. Mchakato mrefu kama huo huo ulitokea katika kuendelezwa kwa fundisho la Sabato ya Biblia, ikiwa ni pamoja na uelewa uliokuwa unaongezeka kwamba Sabato ianze na kuisha wakati wa machweo ya jua. Pia, kutegemeza kazi ya Mungu kifedha kulikubaliwa kwa mara ya kwanza kama utoaji wa mpango mwaka 1859, na kisha, miaka ishirini baadaye, Kanisa la Waadventista wa Sabato wakaanza kutumia mfumo wa zaka uliotokana na Biblia. Njia kama hiyo hiyo ya maendeleo ilitumika katika kumuelewa Mungu wa utatu.

Viongozi wa awali, kama James White na Joseph Bates, waliingiza katika Uadventista uelewa wa Utatu kutoka katika usuli wa madhehebu zao za Kikristo. Kwao Utatu halikuwa fundisho la kibiblia. Waliamini katika "Mungu mmoja aliye hai na wa kweli, Baba mwenyezi . . . Kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu . . . [na] Roho Mtakatifu ni uwezo na nguvu ya Mungu, kwamba mvuto mtakatifu wa Mungu kupitia uwakala wao . . . waovu wanazaliwa upya, wanaongoka na kurejeshwa kwa maisha ya haki na matakatifu" (Joshua Himes, kwenye *Encyclopedia of Religious Knowledge*, ed. J. N. Brown (Battleboro, VT: Fessenden and Co.,

1836), 362, Ilivyonukuliwa kwenye Gerald Wheeler, *James White: Innovator and Overcomer* (Hagerstown, MD: Review and Herald, 2003), 33. *Joshua Himes alikuwa mfuasi wa mafundisho ya Miller katika kikundi cha Christian Connection, wao hawakuamini Utatu, ingawa W. Miller aliamini Utatu).*

Imani hiyo hiyo ilishikiliwa na viongozi wengine wa kanisa, kama Uriah Smith, John Loughborough, John N. Andrews, Dudley Canright, na Joseph H. Waggoner. Merlin Burt anadai kuwa Waadventista wa awali walitaka kuwa waaminifu kwa Biblia si ajabu kwamba wanaposoma mafungu kama "mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote." (Kol. 1:15), au "Mwana pekee wa Mungu" (Yoh. 3:16) wanayabeba kama yalivyo kama lugha ya Kiingereza inavyoyatamka (James White, *"Christ Equal with God,"* Review and Herald, November 29, 1877, 72, imenukuliwa kwa Merlin D. Burt, *CHIS674 Development of Seventh-day Adventist Theology* (Berrien Springs, MI: Center for Adventist Research, Andrews University, 2016), 1195).

Baada ya kikao cha Konferensi Kuu cha Minneapolis mwaka 1888, idadi ya wanateolojia na viongozi wa kanisa, walianza kupokea na kutangaza ujumbe unaohusu uungu wa Yesu. Baadhi miongoni mwa watangulizi walikuwa Alonso T. Jones, William W. Prescott, na Ellet J. Waggoner. Hata wale viongozi waandamizi kama G. I. Butler na U. Smith walibadilisha msimamo wao dhidi ya kupinga utatu, kabla ya mwishoni mwa karne na kuikubali asili ya uungu ya Kristo. Pia katika miisho ya 1890, baadhi ya Waadventista walianza kupaza sauti zao kuhusiana na Roho Mtakatifu kama Nafsi ya Tatu ya Uungu (Godhead). Mmoja wa hao, alikuwa Rufus Underwood, mchungaji na msimamizi kutoka Ohio. Aliandika ifuatavyo: "Roho Mtakatifu ni mwakilishi binafsi wa Kristo kazini . . . Inaonekana kitu cha ajabu kwangu, sasa, kwamba daima nimekuwa nikiamini kuwa Roho Mtakatifu alikuwa tu mshawishi, kulingana na kazi aifanyayo. Lakini tunautaka ukweli kwa kuwa ni ukweli, na tunaukataa uongo kwa sababu ni uongo, bila kujali ni msimamo gani tuliwahi kuwa nao, au ugumu tuliowahi kuwa nao au tulio nao sasa, tunapomwangalia Roho Mtakatifu kama nafsi. Nuru imepandwa kwa ajili ya wenye haki" (Rufus A. Underwood, "The Holy Spirit a Person," *Review and Herald*, May 17, 1898, 310). Hivyo kuanzia 1888, kanisa likahama kwa kasi na kwa uaminifu kutoka "Arianism kuelekea Trinitarianism" (Gary Land, *Uriah Smith: Apologist and Biblical Commentator* (Hagerstown, MD: Review and Herald, 2014), 245).

Katika kipindi cha Kongamano la Biblia cha 1919, William Prescott aliwapa changamoto wahudhuriaji kwa uungu wa milele wa Kristo kupitia mfululizo wa hotuba zake za ibada, lakini haukuwa muda wa waumini wenzake kupokea [jambo] hili. Kwa hiyo, ilichukua miaka mingine mingi hadi Kanisa la Waadventista wa Sabato lilipopokea Utatu katika [mwaka] 1931. Nyaraka za pili na za tatu za Imani za Msingi zilizopitiwa upya zilihusisha Mungu wa utatu mwenye Baba wa milele, Yesu kama Mwana wa Baba wa milele na Mungu mwenyewe, na Roho Mtakatifu kama nafsi ya tatu ya Uungu. Maendeleo haya ya taratibu lakini yanayopiga hatua, yanatoa jibu la swali lenye changamoto la kwa nini Waadventista walikataa kukubali kauli hizi mapema. Kwao, ukweli ni endelevu (Burt, CHIS674 *Development of Seventh-day Adventist Theology*, 209).

## "SURA INAYOMTAMBULISHA MUNGU" (LT 8, 1894)

Mafundisho ya Waadventista wa Sabato hayakuendelezwa kwa sababu Ellen White aliona njozi kwenye somo hili au lile; chanzo [cha mafundisho hayo] kinafuatiliwa nyuma kwenye kujifunza Biblia na uongozi wa Roho Mtakatifu. Hata hivyo, hii isitafsiriwe kumaanisha kuwa alikaa kimya katika maisha na huduma yake. Alikuwa miongoni mwa waasisi, na ukuaji wake wa kiroho ulikua sambamba na ukuaji wa masomo ya Biblia, kama nyongeza ya njozi na ndoto za kiunabii. Kwa mfano, uelewa wake juu ya fundisho la mlango uliofungwa ulikuwa umekua sana kuliko wa wale wengi wa watangulizi wa awali. Mapema 1847, alitangaza kwamba waumini watajishughulisha katika kazi ya umishionari katika kipindi cha mvua ya masika, wakati kazi ya wokovu itakapokuwa inafungwa (EW, 85, 86). Mwaka huo huo alithibitisha kuwa "Mungu bado angali na wafuasi katika makanisa yaliyoanguka ya Babeli" (P. Gerald Damsteegt, *Foundations of the Seventh-day Adventist Message and Mission* (Berrien Springs, MI: Andrews University Press, 1995), 152). Kwa bahati mbaya, wafuasi wenzake hawakuwa katika muafaka na uelewa wa utume wa Ellen White uliokuwa ukikua, na hivyo, wakasita kuufuata.

Kitu cha namna hiyo hiyo kilitokea katika ukuaji wake wa kumwelewa Yesu Kristo ikilinganishwa na uelewa wa Yesu wa Wapingautatu na sehemu kubwa ya Watunzao Sabato na baadaye Waadventista wa Sabato, akiwamo mumewe, James White. Halikuwa kusudi lake kupinga kwa nguvu imani ya watangulizi wa kanisa la Waadventista katika maeneo ambayo hawakuwa tayari kuyapokea. Kulikuwa na mambo mengine muhimu zaidi ya kujadili na kupambana nayo. Kwa hiyo, uelezeaji wa Yesu wa awali wa Ellen White ni wa jumla unaomweleza kiasili. Hatoi maagizo yaliyo ya moja kwa moja kwa Wapingautatu au kwa waumini wa *Semi-Arian*; wala hawapingi viongozi wa kanisa [kwa msimamo wao] juu ya somo hili (George R. Knight, *A Search for Identity: The Development of Seventh-day Adventist Beliefs* (Hagerstown, MD: Review and Herald, 2000), 115).

Baadhi ya maandiko yake ya awali yanamtambulisha Yesu kama nafsi. Kwa mfano miaka inayokaribiana na mwaka 1850 alisema alimwona "Yesu mpendwa kama nafsi." Baada ya kuhojiwa "kumhusu [Yesu] ikiwa Baba Yake alikuwa ni nafsi, na kwamba alikuwa na umbo kama Yeye Mwenyewe. Yesu alisema, 'Nipo katika taswira inayotambulisha nafsi ya Baba Yangu'" (EW, 77). Kadri muda ulivyosogea, maandishi ya Ellen

White yakaanza kumwonesha Yesu katika namna iliyo kamilifu zaidi. Mapema katika miaka ya 1869, alimmweleza kama "mwangaza wa utukufu wa Baba Yake, na utambulisho wa taswira ya nafsi Yake. . . . Alikuwa sawa na Mungu" (2T, 200). Kisha "akaelezea hisia hizo hizo" (Roy Adams, "Divinity of Christ," *The Ellen G. White Encyclopedia*, 691) katika gombo la Shuhuda kwa Kanisa (3T, 566; 4T, 458). Mwaka 1878, alichapisha na kutoa wito kwa wachungaji, ambapo yale maelezo ya jumla ya Yesu yaliondolewa na asili Yake ya umilele ikachukua nafasi hiyo. Hii ilikuwa hatua ya juu sana ya White ya kumwelezea Kristo.

> Watumishi wa Kristo, wanaobeba ujumbe wa kweli kwa watu, kamwe hawawezi kujitumainia au kujiinua ikiwa watakuwa na uoni sahihi wa tabia na kazi ya Kristo, aliye mwanzilishi wa wokovu wa wanadamu. Kutokufaa kwao, udhaifu, na kutokamilika kwa jitihada zao ikilinganishwa na zile za Mwana wa Mungu wa milele, kutawafanya kuwa wanyenyekevu, wasiotumainia nafsi zao, na zitawaongoza kutegemea uwezo na ukamilifu wa Kristo katika kazi zao (RH, August 8, 1878).

Kama miaka tisa baadaye, Ellen White aliwahutubia vijana katika chapisho lake "Yachunguze Maandiko." Mstari wa kwanza kabisa wa chapisho hili unarudia kile alichokisema awali, "Agizo hili ni kutoka kwa Mwana wa Mungu wa milele" (YI, August 31, 1887, 194). Kwake, Mwana wa Mungu alikuwa wa milele na aliye sawa na Mungu. Kufikia wakati huu, alikuwa tayari kuleta mawazo haya nje kwa watu, [bila kujali] kama wapo tayari kusikiliza au la. Hivyo miaka inayofuatia kikao cha Konferensi Kuu cha Minneapolis, mwaka 1888, White alienda mbali zaidi kutoka mtazamo wa kupinga utatu waliokuwa nao wenzake. Kama Moon anavyoielezea, anatambua kwamba "dhana ya kweli ya upatanisho wa Kristo inadai Uuungu wake wa milele kwa ukamilifu" (Jerry Moon, "The Quest for a Biblical Trinity: Ellen White's 'Heavenly Trio' Compared to the Traditional Doctrine," *Journal of the Adventist Theological Society*, 17(Spring 2006), 149).

Kuanzia mapema 1890, maandiko ya mjumbe wa Mungu yanafunua uzuri wa Kristo katika machapisho [yake] mengi. Kati *Signs of the Times*, anaandika kwamba "Maneno ya Kristo yalikuwa na maana nzito na kamilifu alipotoa madai kuwa yeye na Baba walikuwa umoja wakifanana kwa tabia" (ST, November 27, 1893, 80). Mnamo 1897, alitangaza kwamba Yesu "alikuwa sawa na Mungu, asiye na mwisho na mwenye uwezo wote . . . Yeye ni Mwana wa milele, mwenye uzima wake mwenyewe" (Ms 101, 1897). Hata hivyo, ufafanuzi huu ni baadhi tu kati ya mawazo yake aliyoyaandika na kuyachapisha katika kitabu cha *Tumaini la Vizazi Vyote*. Kazi hii bora kuhusiana na maisha ya Yesu ina mikusanyiko ya njozi na maandiko ya awali ya Ellen White, pamoja na masomo ya Biblia [yaliyopangiliwa] kwa uangalifu "ikifuatiwa na matumizi ya rejea zingine" (Jerry Moon, "The Desire of Ages," *The Ellen G. White Encyclopedia*, 764). Uungu wa milele wa Kristo umeoneshwa kikamilifu kupitia kurasa za kitabu hiki. Ingawa ilichukua idadi ya miaka mingine michache kwa waumini kuuelewa kikamilifu Ujumbe, kitabu hiki [*Tumaini la Vizazi Vyote*] kikawa chanzo cha uelewa wa jumla wa Waadventista kuhusiana na nafsi tatu za Uungu. Ni muhimu kutaja hapa kuwa, licha ya ukweli kwamba kuna baadhi ya waumini wanaodhani wasaidizi wa Ellen White, aliowatumia kukiandaa na kukichapa kitabu cha *Tumaini la Vizazi Vyote*, walichomeka mtazamo wao na kuchapa mawazo yao katika kitabu hiki, Ellen White mwenyewe ndiye aliyekihariri na kulipia uchapishaji wake" (Burt, *CHIS674 Development of Seventh-day Adventist Theology*, 205). Hivyo madai yao hayakuwa halali. Kwa nyongeza, Tim Poirier alifanya utafiti wa kina juu ya somo hili na kugundua "kwamba mswaada wa maandishi ya mkono wa awali, nakala zilizoidhinishwa, na/au matoleo ya kwanza ya kazi yake iliyochapishwa vinaunga mkono maelezo ya Utatu yanayopatikana leo kwenye maandiko yake" (Tim Poirier, "Ellen White's Trinitarian Statements: What did She Actually Write?" *Ellen White and Current Issues Symposium* (Berrien Springs, MI: Center for Adventist Research, Andrews University, 2006), 2:38, 39).

Karibu na kuvuka kwa karne maandiko yake yakawa yamejengwa kikamilifu juu ya Kristo. Machapisho ya White, kama vile, *Njia Salama* (1892), *Mlima wa Baraka* (1896), *Christ's Object Lessons* (1900), *Huduma ya Uponyaji* (1905), *Matendo ya Mitume* (1911), na mengine mengi, yanafunua uelewa mpana wa picha ya Yesu. Yanapigia chapuo siyo tu asili ya milele ya Mwokozi wa ulimwengu, bali pia udhihirisho wa kuwa na uzima wake mwenyewe [usioazimwa] "wenye ukamilifu wa Uungu" (SpT"B," No. 7, 62, 1906; Ev, 614). Uungu wake uliorudiwa mahali pengi na kwa namna nyingi, unaelezea Yesu ni nani: "Kristo alikuwa Mungu kimsingi, na katika kiwango cha juu. Alikuwa pamoja na Mungu tangu milele, Mungu aliye juu ya yote, aliyebarikiwa milele" (RH, April 05, 1906, 227).

*Watumishi wa Kristo, wanaobeba ujumbe wa kweli kwa watu, kamwe hawawezi kujitumainia au kujiinua ikiwa watakuwa na uoni sahihi wa tabia na kazi ya Kristo*



**“KADRI ALIVYO NAFSI NA MUNGU NI NAFSI" (Ms 66, 1899; Ev 615).**

Mnamo miaka hamsini ya kwanza ya Huduma yake, Ellen White alibaki kuwa na msimamo wa Biblia (Burt, *CHIS674 Development of Seventh-day Adventist Theology*, 200) kuhusiana na nafsi ya Roho Mtakatifu. Alijiondoa katika kuandika kuhusu somo hili “kwa uwazi kamili” (Ibid.). Jukumu lake la kiunabii halikuwa kutambulisha chochote kilicho kipya, bali kuelekeza usikivu wa watu kwa Biblia. Kama Jerry Moon anavyoshauri, hakuhoji Roho Mtakatifu. Wakati huo huo, mnamo 1858 alimuunganisha Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu katika kisa cha ubatizo wa Kristo. Wakati huo huo aliepuka kutaja “Roho Mtakatifu kuhusiana na mabaraza ya kiungu yanayohusu uumbaji na mpango wa wokovu . . . [machapisho yake] Yangeweza kusomwa bila mgongano na Waadventista watangulizi wote bila kujali mafunzo yao ya utatu au yale yanayopinga utatu” (Jerry Moon, “The Adventist Trinity Debate, Part 2: The Role of Ellen G. White,” *Andrews University Seminary Studies*, 41(2003), 281). Na huo ndio uliokuwa msimamo wake kuhusu somo hili kwa idadi ya miaka.

Hata hivyo, miaka [kadhaa] baadaye, wakati ndugu Chapman alipomlinganisha Roho Mtakatifu na malaika Gabrieli, White ilimbidi ajibu kwa kauli ifuatayo:

> Asili ya Roho Mtakatifu ni fumbo; halijafunuliwa kwa dhahiri, na huwezi kulielezea kwa wengine, kwa kuwa Bwana hajalifunua kwako . . .
>
> Si lazima kujua na kuweza kufafanua vile Roho Mtakatifu alivyo. Kristo anatuambia kwamba Roho Mtakatifu ni Mfariji, na Mfariji ni Roho Mtakatifu, “Roho wa kweli, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu.” [Yohana 14:26] . . . Hii inafanya rejea kwa Roho wa Kristo aliye mahali pote, anayeitwa Mfariji” (Lt 7, 1891).

Ellen White alitoa kauli iliyopiga hatua kubwa sana kuhusu Roho Mtakatifu, mwaka 1893, “Anamfanya Kristo kuwa nafsi hai, na bado [yeye] ni nafsi iliyo tofauti” (Ms 93, 1893). Hata hivyo, kwenye mstari unaofuata tu, anamtaja kwa jina lisilohusisha nafsi: “Tunaweza kuwa na Roho Mtakatifu ikiwa tutaiomba” (Ibid.). Alikuwa na mtazamo huo huo hata miaka kadhaa mbele. Mwaka 1900, akifafanua kisa cha ngano na magugu, alisema: “Ni kweli, Roho Mtakatifu ameenda ulimwenguni mwote, kila mahali inatembea mioyoni mwa watu” (COL, 70). Kwa utafiti mdogo, mtu anaweza kuhitimisha kuwa White alimfanya Roho Mtakatifu kuwa nafsi, kwa sehemu kidogo tu. Hata hivyo, hilo halikuwa swala muhimu. Wakati mara chache alikuwa akitumia nomino isiyohusiana na nafsi “i,” pia alitumia “a” kabla ya mwaka 1890 na baada ya hapo. Kwa mfano, mwaka 1884 aliandika: “Roho Mtakatifu anamwinua na kumtukuza Mwokozi.

Ni ofisi yake ndiyo inayomtambulisha Kristo . . . Roho wa kweli ndiye mwalimu pekee mwenye uwezo wa kiungu; wale wanaofundishwa naye wameingia katika shule ya Kristo.” (ST, April 3, 1884, 422) Miaka michache baadaye, alianza kutumia kiwakilishi nafsi “A” ikiwa na herufi kubwa. Ukweli huu unashuhudia ukuaji wake wa uelewa wa somo. Hivyo, mnamo 1906 aliandika: “Roho Mtakatifu ni nafsi . . . Roho Mtakatifu anayo nafsi, vinginevyo asingeweza kushuhudia kwenye roho zetu na kupitia roho zetu kwamba tu watoto wa Mungu. Ni lazima pia atakuwa nafsi ya uungu, vinginevyo asingeweza kuchunguza siri zilizofichika katika akili ya Mungu” (Ms 20, 1906: Ev, 616).

Kwenye kitabu chake T*umaini la Vizazi Vyote*, White kwa kurudia rudia anamrejea Roho Mtakatifu kwa kiwakilishi nafsi “A.” Zaidi ya hayo, anatambulisha kwa wasomaji kauli yenye ushawishi na msukumo ambapo anawekea herufi kubwa kifungu chote kinachohusu Roho Mtakatifu: “Roho alikuwa achukuliwe kama wakala ahuishaye, na bila huyu kafara ya Kristo isingekuwa na faida . . . Dhambi ingeweza kuzuiwa na kuishindwa kupitia kwa wakala mwenye uwezo wa nafsi ya tatu ya Uungu, ambaye angekuja akiwa hana nguvu zilizoboreshwa, bali akiwa na ukamilifu wa uweza wa kiungu” (DA, 671).

White anatambua ukweli kwamba kazi ya Roho Mtakatifu ni ya kina na

inayohitaji umakini, lakini matokeo ya Huduma Yake yanaonekana katika maisha ya waumini wake. Kwa hiyo, anamuelezea kama Mwelimishaji, (CT, 37, 38) anayethibitisha kuwepo kwa dhambi na "anayeiondoa kutoka moyoni kwa idhini ya mawakala wa kibinadamu" (ML, 43). Hubadilisha maisha (DA, 172) na huchukua nafasi muhimu katika utume wa kanisa. (RH, March 19, 1895, 239, 240; Ev, 701). Katika maandiko yake, White anatofautisha baina ya "udhihirisho wa kimakosa na wa kiukweli wa Roho (Karen K. Abrahamson and John T. Baldwin, "Holy Spirit," *The Ellen G. White Encyclopedia*, 875) katika matukio ya siku za mwisho." Kwake [Ellen White] "kelele tupu na kupiga mayowe siyo ushahidi wa utakaso, au kushuka kwa Roho Mtakatifu . . . Vitendo vya vurugu vinaunda tu maruweruwe kwenye akili za waumini" (2SM, 35). Pia anaweka wazi jukumu la Roho Mtakatifu kwa matukio ya siku za mwisho katika maandalizi ya Kuja kwa Kristo mara ya pili. Mfano wa jambo hili waweza chukuliwa kutoka katika *Matukio ya Siku za Mwisho*.

> Mvua ya masika, itakayonyesha karibu na kufungwa kwa msimu, huyaivisha mazao na kuyatayarisha kwa kuvunwa. Bwana hutumia utendaji huu wa asili kuwakilisha kazi ya Roho Mtakatifu. Kadri umande na mvua vinavyokuwa vya kwanza kusababisha mbegu kuota, na kisha kuivisha mazao, ndivyo na Roho Mtakatifu anavyoendelea kutoka hatua moja hadi nyingine, mchakato wa ukuaji wa kiroho. Kuiva kwa mazao kunawakilisha ukamilifu wa kazi ya neema ya Mungu mioyoni. Tunapaswa sote kubadilishwa tufanane na Kristo (LDE, 183; TM, 506).

Hivyo, kupitia maisha yake ya huduma ya matamko na uandishi, Ellen White anamfafanua Roho Mtakatifu kupitia mtazamo wake wa kina uliokua wa nafsi ya tatu ya Uuungu. Kwa kweli, anaandika kwa namna iliyo rahisi na ya wazi juu ya "unafsi wa Roho Mtakatifu, kuliko mwandishi mwingine ye yote wa wakati wake." (Burt, *CHIS674 Development of Seventh-day Adventist Theology*, 203) Hiyo ndiyo sababu anawaalika waumini" kushirikiana na mamlaka tatu kuu za mbinguni, – Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, – na mamlaka hizi zitatenda kazi kupitia kwetu, na kutufanya watendakazi pamoja na Mungu (Lt 253a, 1903; Ev, 617).

*Roho wa kweli ndiye mwalimu pekee mwenye uwezo wa kiungu; wale wanaofundishwa naye wameingia katika shule ya Kristo*

## UTATU

Tukizungumzia kuhusu Utatu, mtu hawezi akapata neno "Utatu" katika maandiko ya Ellen White. Ingawa kunaweza kuwepo sababu nyingi kwa nini hakutumia neno hili, sababu kuu inaweza kuhusiana na mwitikio wake juu ya mgogoro wa wale wasioamini kama Mungu ni nafsi (pantheistic), na uelewa wa wakati huo wa Utatu vikiunganishwa na dhana mbalimbali za kifalsafa zilizoanza karne ya ishirini (Moon, "Godhead," *The Ellen G. White Encyclopedia*, 844). "Uwakilisho wa kiroho wa Mungu kwa kutumia vielelezo vya nuru na maji" vilivyofanywa na Dr. J. H. Kellogg, "vilijengwa juu ya dhana ya filosofia ya Kiyunani" (Woodrow Whidden, Jerry Moon, and John W. Reeve, *The Trinity: Understanding God's Love, His Plan of Salvation, and Christian Relationships* (Hagerstown, MD: Review and Herald, 2002), 217, 219). Ellen White alipinga kwa nguvu mafundisho ya Kellog juu ya somo hili. Mwaka 1905 akaandika yafuatayo:

> "Viwakilishi hivi vyote vya kiroho havina maana yoyote. Si vikamilifu na havina ukweli. Vinadhoofisha na kupunguza Ukuu ambao hakuna mfanano wowote wa kidunia unaoweza kulinganishwa nao. Mungu hawezi kufananishwa na vitu ambavyo mikono Yake imeviumba. Hivi ni vitu vya kidunia tu, vinavyoteseka chini ya laana ya Mungu kwa sababu ya dhambi za mwanadamu. Mungu hawezi kuelezwa kwa kutumia vitu vya kidunia. Baba ndiye ukamilifu wa Uungu wote katika hali ya mwili, na anayeonekana na macho ya [wanadamu] wanaokufa (*Testimonies for the Church Containing Messages of Warning and Instruction to Seventh-day Adventists*, 62; "Come Out and Be Separate," Ev, 614).

Licha ya ukweli kwamba alikuwa hatumii neno Utatu, Ellen White kwa kurudia rudia alizielezea Nafsi za Uungu kwa maneno mengine. Mahali pengi alilieleza neno hili kwa [kusema] "nafsi tatu hai za utatu wa mbinguni" (Ms 21, 1906). Pia huandika kuwahusu kama "mamlaka za ukuu wa juu sana za mbinguni" (Lt 253a, 1903; Ev, 617) na "viongozi wa milele wa mbinguni" (Ms 130, 1901; Ev, 616). Maandiko yake kwa uwazi kabisa "uwingi na umoja" utatu

na umoja – mambo ya msingi ya uelewa rahisi wa kibiblia wa Utatu" (Whidden, Moon, and Reeve, 198). Zaidi sana, anasisitiza asili zao kama nafsi zenye kuhusiana na anauelezea umoja wao [kuwa upo] katika asili, tabia, kusudi, na upendo (Moon, "Godhead," The *Ellen G. White Encyclopedia*, 844). Na katika kufafanua analinganisha umoja wa mbinguni na utengamano wa Kristo na wanafunzi wake, ambao hauharibu utambulisho wao. Kisha anasema, "ni wamoja katika kusudi, nia, tabia, lakini si katika nafsi. Hivi ndivyo ambavyo Mungu na Kristo ni umoja" (MH, 422).


Tukiangalia maandiko yote ya Ellen white, mtu anaweza kuona mwendelezo wa uthibitisho wa Mungu mwenye Utatu, kwake, Yesu si kiumbe aliyeumbwa; anao uzima ulio sawa na wa Baba. Mwaka 1888, Ellen White alithibitisha kuwa upatanisho wake unahitaji Uungu Wake Mkamilifu (GC, 524). Baadaye, miaka ya 1890 alitambua upekee na hali ya kuwa nafsi kwa Roho Mtakatifu (Lt 8, 1896). Ndipo kwenye 1905, bila kigugumizi anatangaza Imani yake katika "nafsi tatu za uungu zilizoungana kuwa Mungu mmoja"(Jerry Moon, "The Adventist Trinity Debate, Part 2: The Role of Ellen G. White," *Andrews University Seminary Studies*, 41(2003), 290). Baada ya utafiti wake wa kina juu ya somo hili, Moon kwa wazi kabisa anahitimisha kwamba, "Kuna maendeleo yaliyo dhahiri kutoka kwa yaliyo rahisi kwenda kwa yenye utata, akishauri kuwa uelewa wa Ellen White ulikuwa na kubadilika kwa kadri alivyokuwa akipokea nuru ya ziada" (Ibid., 284).




## FUMBO LA UTATU

Mada iliyojadiliwa kifupi, ya Mungu mwenye Utatu ni yenye kina kwa asili yake, yenye upana kwa utendaji wake, na yenye kimo katika ukuu wake, ngumu kwa mwanadamu kuielewa kikamilifu au kuitolea maelezo yanayoshawishi akili. Ndiyo sababu, katika kuhitimisha kazi hii, ni muhimu kuonesha ukweli juu ya ukomo wa akili ya kibinadamu katika kulielewa somo lililofunuliwa na Biblia na kuwasilishwa na nabii wa Mungu. Wakati Ellen White hatua kwa hatua akimfunua Mungu wa Utatu, anatambua kuwa asili yenye ukuu ni fumbo. Awali ya yote, anaandika kwamba, "Kusudi la Mungu ni kujificha zaidi kuliko anavyoweza kujidhihirisha kwa wanadamu" (Ms 4, 1882). Pili, kufanyika mwanadamu kwa Yesu Kristo ni "fumbo kubwa, fumbo ambalo halitafahamika kikamilifu, na kueleweka kikamilifu katika ukuu wake wote hadi kunyakuliwa kwa watakaokombolewa kutakapotokea" (Lt 280, 1904). Hayo hayo yanasemwa kuhusu Nafsi ya Tatu ya Uungu, kuhusiana na asili Yake, "ni fumbo. Mwanadamu hawezi kulielezea, kwa kuwa Bwana hajalifunua kwao" (AA, 52). Hivyo, wakati watu wa Mungu hawawezi kuuelewa Utatu au hata kwa uchache kutambua ukamilifu wake, wanapaswa kuwapokea hawa "wenye nafsi tatu hai wa utatu wa mbinguni" kwa imani iliyo hai, kwa sababu "mamlaka hizi zitashirikiana na viumbe watii wa mbinguni katika jitihada zao za kuishi maisha mapya katika Kristo" (Ev, 615).

Nakala hii imefupishwa kutoka kwa: Galeniece, Anna M. "The Heavenly Trio in Ellen White's Writings." In *The Trinity and the Bible*, edited by Eriks Galenieks, 185-205. Nairobi: Adventist Theological Society - Adventist University of Africa Chapter, 2018





# Makala ya Watoto

Heri ya Mwaka Mpya!
Tunaanza mwaka huu kwa kujifunza kuhusu Mungu. Chemsha bongo ifuatayo ina majina tofauti ya Mungu na mambo mengine yanayohusiana na Mungu. Yatafute majina hayo kisha ujifunze zaidi kuhusu majina hayo kwa kusoma Biblia na Roho ya Unabii. Kumbuka kuwaambia wengine ulichojifunza.

P V U
J F A W I U P F O
Q A H X X Q X L S G E C S
U N H X Z B Z A H L L D V L I H S
U N H P E Z B W H C M F K F F B C G N
J K J Z A N U W T N Z M A I F R P D I A A
L F K W B B D C G B D K P P U U Y I W P I
O P G U M N M A F O O H X V C X L E B D T K R
P K Y O Y U F I A K A Z B Y I J K Q T K Q N Y
L J X G J P B Z V L D Z Q C M Q L L V I W A P O E
X N Y D R N U R D D E U N B U U Y T H P A C H V N
Z B Y M U G N U M X O L M V U X K E V U X B I J O
M X M Z B B D G Q V Y C E E G M C K M S I N J A I R D
F A P M U W I A H M U R E X N B O Q M E U A A I B M N
A P Q F B Z U N C V Q Z T U V A P U Q J O D Z J Z N G
W J E A I M G G Z D R F J T J G O H T G E I M X M
L K E U K Z R V U F E N F R I C Z M R M T W Y K N
E F U Y J N O W N N M R U S B P E K S B M Q O Q X
I G E H K C K K T I F T C T B U Y I F A M J F
H Z Y G M T G O Q A N A W M W P R P Y B V Y F
O I S Z M B G W U Q T R U D T C K O K N A
O K Z P K J Q J M M U T I K F P Z G Z I D
J M D U O I F P U B G L J G I C L Q U
T V J V M W N Y H C B Q I X Q D V
Z O O H O R G K E V V R Q
X A X H V Z E U H
W Q Z

Mbinguni | Yesu | Mwana | Mungu | Baba | Roho | Muumbaji
Mwokozi | Utatu | Mkombozi | Mfariji | Mtoaji | Milele




Idara ya Uchapishaji kutoka Kanisa la Kiadventista la Laiser Hill wakati wa ziara yao katika Ofisi ya Tawi ya E. G. White

Tutembelee katika
Adventist University of Africa
Advent Hill, Barabara ya Magadi, Ongata Rongai, Kenya

www.aua.ellenwhite.org
www.egwwritings.org

Ellen G. White Estate Branch Office - AUA

egweboaua

Ili uweze kupokea *Mambo Muhimu* kwa Kiingereza au *Swahili*, tuma ombi kwa **egwebo@aua.ac.ke** au utupigie simu kwa **+254-733-333-451/2**

**Vituo vya Utafiti vya Ellen G. White barani Afrika**

**ECD: University of Eastern Africa - Baraton,**
Eldoret, Kenya
egwrc@ueab.ac.ke

**SID: Helderberg College,**
Cape Town, South Africa
clarkec@hbc.ac.za

**WAD: Babcock University,**
Ilishan Remo, Ogun State, Nigeria
egwsdarc@babcock.edu.ng